HAKI ZA MSINGI ZA BINADAMU KWA WAFUNGWA WA MATAIFA YA KIGENI (FNPs)

Maelezo

1. Haki ya kupokea maelezo ya haki zako na jinsi ya kupata haki hizo kwa lugha ambayo unaelewa wakati unapokamatwa na wakati wa kutiwa nguvuni au kuanza kifungo chako, au mara moja baadaye. (UN Principles 13-14, CoE Police 55)

2. Haki ya kufahamishwa kuhusu sababu za kukamatwa na za mashtaka kwa lugha ambayo mfungwa anaelewa. (ICCPR 14.3, UN Principles 10, EU2012 6)

3. Haki ya kumfahamisha mtu unayemchagua kuhusu kukamatwa kwako. (UN Principle 16.1, CoE FNP 15.2, CoE Police 57, EU2012 4.2 c)

4. Haki ya kupokea maelezo kuhusu sheria za gereza na haki na majukumu ya wafungwa kwa lugha ambayo mfungwa anaweza kuelewa. (UN Rec 4, SMR 54-55, EPR 30.1, CoE FNP 15.1)

5. Haki ya kufahamishwa kuhusu haki za kibalozi, za kuwasiliana na mamlaka ya ubalozi na kuweza kutembelewa na kupokea usaidizi wa ubalozi. (VCCR 36.1 b-c UN Principles 16.2, UN Res (e), UN Rec 4, SMR 62, CAT 6.3, EU Charter 46, EPR 37.1, CoE FNP 24)

6. Haki ya kufahamishwa kuhusu uwezekano wa kurejeshwa nchi yako ya asili. (EPR 37.5, CoE FNP 15.3, CoE Transfer 4.1, EU909JHA 6.4)

Kesi ya haki

7. Haki ya kupata matibabu yanayofaa na kesi ya haki. Kila mtu ambaye ameshtakiwa atachukuliwa kuwa hana hatia hadi adhibitishwe kuwa na hatia kwa mujibu wa sheria. (ICCPR 14, UDHR10-11.1, ECHR 6, EU Charter 46-47)

8. Haki ya kupokea usaidizi wa kisheria katika mashtaka ya jinai. (ICCPR 14.3 d, SMR 61, UN Principles 17-18, EPR 23, CoE FNP 21)

9. Haki ya kupokea usaidizi bila malipo wa mkalimani wakati mfungwa hawezi kuelewa au kuongea lugha inayotumiwa mahakamani. (ICCPR 14.3 f, UN Principles 14, UN Res (c))

10. Haki ya usawa mbele ya mahakama na kushtakiwa bila kucheleweshwa. (ICCPR 14.1, 14.3 c)

11. Haki ya kuachiliwa na kusubiri kesi, isipokuwa mahakama au mamlaka mengine yaamue kivingine kwa mujibu wa utekelezaji wa haki. (UN Principle 39, CoE FNP 5)

12. Haki ya kuhukumiwa au kuwekewa vikwazo sawa kama watuhumiwa wengine. (UN Rec 2, UN Res (d), CoE FNP 4, 14.1)

13. Haki ya kutopewa adhabu kali kifungoni au kupata hali mbaya gerezani kwa sababu ya kuwa mfungwa wa kigeni. (UN Res (b))

14. Haki ya kuweza kuzingatiwa kikamilifu kuachiliwa mapema. (CoE FNP 6)

Matibabu

15. Haki ya kutendewa kama mwanadamu na kwa heshima ya uutu wa mwanadamu. (ICCPR 10.1, UDHR 5, SMR 1, CAT 1-2, UN Basic Principles 1, ECHR 3, EU Charter 4, EPR 1)

16. Haki ya kulindwa dhidi ya mateso au utendewaji au adhabu ya unyama au udhalilishaji. (ICCPR 7, UDHR 5, CAT 7, ECHR 3, EU Charter 4)

17. Haki ya kutendewa kwa njia ambayo inazingatia hali na mahitaji mahsusi ya kibinafsi ya wafungwa wa mataifa ya kigeni. (CoE FNP 3)

18. Haki ya kutobaguliwa (pamoja na misingi kama ile ya uasili wa kitaifa na lugha) na kupokea ulinzi thabiti dhidi ya ubaguzi. (ICCPR 26, UDHR 7, SMR 2, UN Principles 5, UN Basic Principle 2, EU Charter 21-22, EPR 13, CoE FNP 7)

19. Haki ya kupata huduma ile moja ya afya na mipango ya matibabu ambayo inapatikana kwa wafungwa wengine. (EU Charter 35, CoE FNP 31)

20. Haki ya uhuru wa mawazo, dhamira na dini na uhuru wa kudhihirisha hii katika kuabudu na katika maadhimisho. (ICCPR 18.1, UDHR 18, SMR 65-66, UN Basic Principles 3, UN Rec 3, EU Charter 10.1, EPR 29, CoE FNP 30)

21. Haki ya kuvaa mavazi na kudumisha usafi wa kibinafsi kwa njia ambayo haikosei utamaduni au hali za kidini za wafungwa na kupata chakula ambacho kinazingatia mahitaji ya kitamaduni na kidini. (UN Rec 4, CoE FNP 18,19)

22. Haki ya kutotatizwa faraghani, haki ya kuwa na familia na kuweza kuwasiliana mara kwa mara (pia kupitia kutembelea) na familia na marafiki. (ICCPR 17, UDHR 12, SMR 58, UN Rec 5, EU Charter 7, EPR 24, CoE FNP 22)

23. Haki ya kupokea huduma za ukalimani na utafsiri gerezani na uwezekano wa kujifunza lugha ili kuwezesha mawasiliano. (SMR 61.2, EPR 38.3, CoE FNP 8, 29.1)

24. Haki ya kupata elimu, kazi, na mafunzo ya kikazi kama wafungwa wale wengine wa nchi hii. (UN Rec 1, SMR 4.2, 71, EPR 26, 28, CoE FNP 27.1, 29)

25. Haki ya kuwasilisha ombi au kulalamika bila kukaguliwa, kwa msimamizi mkuu wa gereza, mamlaka ya mahakama au mamlaka mengine yanayostahili kupitia njia zilizoidhinishwa. (SMR 56, UN Rec 4, EPR 70)

Makazi mapya

26. Haki ya kutendewa kwa njia ambayo inalenga kubadilisha na kurekebisha tabia ili kukuandaa kurejea katika jamii. (ICCPR 10.3, SMR 4, EPR 6, 107, CoE FNP 9, 29.2, 35)

27. Haki ya kufahamishwa mapema kuhusu hali zako za kisheria baada ya kuwekwa huru. (CoE FNP 35.2 a)

28. Haki ya kulindwa dhidi ya kufukuzwa, kurudishwa ('kwa lazima') au kurejeshwa nchi ambayo ina hatari kubwa ya kupata hukumu ya kifo, mateso au utendewaji au adhabu nyingine za unyama au udhalilishaji. (UDHR 14, CAT 3, EU Charter 19.2)

29. Haki ya ridhaa na uwezo wa mfungwa kujumuishwa katika jamii kuzingatiwa katika uamuzi wa kumhamisha hadi nchi nyingine. (UN Transfer 1, CoE Transfer 4, CoE FNP 10)

30. Haki ya kuanzisha mahusiano na mawakala wa nje ili kupokea usaidizi na msaada wa makazi mapya baada ya kuwekwa huru. (SMR 107-108, 81, EPR 107, CoE FNP 37, CoE Probation 64)

Umoja wa Mataifa

- Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR)
- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR)
- Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Mateso (CAT)
- Sheria Wastani za Kuwatendea Wafungwa (SMR Mandela Rules)
- Mkataba wa Vienna kuhusu Mahusiano ya Ubalozi (VCCR)
- Mfano wa Makubaliano ya Kuwahamisha Wafungwa Wageni (UN Transfer)
- Kanuni Msingi za UN za Kuwatendea Wafungwa (UN Basic Principles)
- Kanuni za UN za Kuwalinda Watu Wote walio katika Kifungo au Gereza ya Aina Yoyote ((UN Principles)

- Mapendekezo kuhusu jinsi ya Kuwatendea Wafungwa wa Kigeni (UN Rec)
- Azimio la UN la 1998/22 Hali ya Raia wa Kigeni katika kesi za jinai ((UN Res)

Baraza la Ulaya

- Mkutano wa Uropa wa Haki za Binadamu (ECHR)
- Sheria za Gerezani za Ulaya (EPR)
- Mapendekezo (2012)12 kuhusu wafungwa wa kigeni (CoE FNP)
- Mkutano wa Uhamisho wa Watu Waliofungwa (CoE Transfer)
- Mapendekezo CM/Rec(2010)1 Sheria za Majaribio (CoE Probation)
- Mapendekezo Rec(2001)10 Kanuni ya Maadili Meka ya Polisi wa Ulaya (CoE Politics)

Umoja wa Ulaya

- Mkataba wa Haki za Msingi za Umoja wa Ulaya (EU Charter)
- Uamuzi wa Mfumo wa Baraza 2008/909/JHA (EU909JHA)
- Maagizo 2010/64 kuhusu haki za ukalimani na utafsiri katika kesi za jinai (EU2010)
- Maagizo 2012/13 kuhusu haki za maelezo katika kesi za jinai (EU2010)